# Hosea

1 Neno la Mwenyezi Mungu lililomjia Hosea
mwana wa Beeri wakati wa utawala wa Uzia,
Yothamu, Ahazi na Hezekia, wafalme wa Yuda,
na wakati wa utawala wa Yeroboamu mwana wa
Yehoashi, mfalme wa Israeli.

*Mke wa Hosea na watoto wake*

2 Mwenyezi Mungu alipoanza kuzungumza
kupitia Hosea, Mwenyezi Mungu alimwambia,
"Nenda ukajitwalie mwanamke wa uzinzi na
watoto wa uzinzi, kwa sababu nchi ina hatia ya
uzinzi wa kupindukia kwa kumwacha Mwenyezi
Mungu."
3 Kwa hiyo alimwoa Gomeri binti Diblaimu,
naye akachukua mimba na kumzalia Hosea
mwana.
4 Kisha Mwenyezi Mungu akamwambia Hosea,
"Mwite jina Yezreeli*, kwa kuwa kitambo kidogo
nitaiadhibu nyumba ya Yehu kwa ajili ya mauaji
ya kule Yezreeli, nami nitaukomesha ufalme wa
Israeli.
5 Katika siku ile nitavunja upinde wa Israeli
katika Bonde la Yezreeli."
6 Gomeri akachukua tena mimba akamzaa
binti. Kisha Mwenyezi Mungu akamwambia
Hosea, "Mwite Lo-Ruhama†, kwa maana sitaone-
sha tena upendo kwa nyumba ya Israeli, kwamba
nisije kabisa nikawasamehe.

---

* **1:4** maana yake *Mwenyezi Mungu hupanda* † **1:6** maana yake *Sio mpendwa wangu*

7 Hata hivyo nitaonesha upendo kwa nyumba
ya Yuda, nami nitawaokoa si kwa upinde, upanga
au vita, wala kwa farasi na wapanda farasi, bali
kupitia Mwenyezi Mungu, Mungu wao."
8 Baada ya Gomeri kumwachisha Lo-Ruhama
kunyonya, Gomeri alipata mwana mwingine.
9 Kisha Mwenyezi Mungu akasema, "Mwite Lo-
Ami‡ kwa maana ninyi si watu wangu, nami si
Mungu wenu.
10 "Hata hivyo Waisraeli watakuwa kama
mchanga kando ya bahari, ambao hauwezi
kupimika wala kuhesabiwa. Mahali pale
walipoambiwa, 'Ninyi si watu wangu,' wao
wataitwa 'wana wa Mungu aliye hai'.
11 Watu wa Yuda na watu wa Israeli
wataunganishwa tena, nao watamchagua
kiongozi mmoja nao watakwea watoke katika
nchi, kwa kuwa siku ya Yezreeli itakuwa kuu
sana.

# 2

1 "Waambie ndugu zako, 'Watu wangu,' na pia
waambie dada zako, 'Wapendwa wangu.'

### *Israeli kuadhibiwa na kurudishwa*

2 "Mkemeeni mama yenu, mkemeeni,
kwa maana yeye si mke wangu,
nami si mume wake.
Aondoe sura ya uzinzi katika uso wake
na uzinzi kati ya matiti yake.
3 Kama sivyo nitamvua nguo zake awe uchi
na kumwacha uchi kama siku ile aliyozaliwa.
Nitamfanya kama jangwa,

‡ **1:9** maana yake *Sio watu wangu*

nitamgeuza awe nchi ya kiu,
nami nitamuua kwa kiu.
4 Sitaonesha upendo wangu kwa watoto wake,
kwa sababu ni watoto wa uzinzi.
5 Mama yao amekosa uaminifu
na amewachukua mimba katika aibu.
Gomeri alisema, ‘Nitawaendea wapenzi wangu,
ambao hunipa chakula changu
na maji yangu,
sufu yangu na kitani yangu, mafuta yangu
na kinywaji changu.’
6 Kwa hiyo mimi Mungu nitaizuia njia yake
kwa vichaka vya miiba,
nitamjengea ukuta ili
asiweze kutoka.
7 Gomeri atawafuatia wapenzi wake lakini hatawapata;
atawatafuta lakini hatawapata.
Kisha atasema,
‘Nitarudi kwa mume wangu kama kwanza,
kwa maana nilikuwa na hali njema
kuliko sasa.’
8 Gomeri hajakubali kuwa mimi ndiye
niliyempa nafaka, divai mpya na mafuta,
niliyemwongezea fedha na dhahabu waliyoitumia
kwa kumtumikia Baali.

9 “Kwa hiyo nitachukua nafaka yangu wakati itakapokomaa
na divai yangu mpya wakati itakapokuwa tayari.
Nitamnyang’anya sufu yangu na kitani yangu
iliyokusudiwa kufunika uchi wake.

10 Basi sasa nitaufunua ufisadi wake
mbele ya wapenzi wake;
hakuna yeyote atakayemtoa
mikononi mwangu.
11 Nitakomesha furaha na macheko yake yote:
sikukuu zake za mwaka,
sikukuu za Miandamo ya Mwezi,
siku zake za Sabato,
sikukuu zake zote zilizoamriwa.
12 Nitaiharibu mizabibu yake na mitini yake,
ambayo alisema yalikuwa malipo yake
kutoka kwa wapenzi wake;
nitaifanya kuwa kichaka,
nao wanyama pori wataila.
13 Nitamwadhibu kwa ajili ya siku
alizowafukizia uvumba Mabaali;
alipojipamba kwa pete
na kwa vito vya thamani,
na kuwaendea wapenzi wake,
lakini mimi alinisahau,"
asema Mwenyezi Mungu.

14 "Kwa hiyo sasa nitamshawishi;
nitamwongoza hadi jangwani
na kuzungumza naye kwa upole.
15 Huko nitamrudishia mashamba yake ya mizabibu,
nami nitalifanya Bonde la Akori*
mlango wa matumaini.
Huko ataimba kama alivyofanya katika siku za ujana wake,
kama siku zile alizotoka Misri.

---

* **2:15** yaani *Bonde la Taabu*

16 “Katika siku ile,” asema Mwenyezi Mungu,
“utaniita mimi ‘Mume wangu†’;
hutaniita tena mimi ‘Bwana wangu‡.’
17 Nitaondoa majina ya Mabaali kutoka mdomoni mwake,
wala hataomba tena kwa majina yao.
18 Katika siku ile nitafanya agano kwa ajili yao
na wanyama wa kondeni, na ndege wa angani,
na viumbe vinavyotambaa ardhini.
Upinde, upanga na vita,
nitaondolea mbali katika nchi,
ili wote waweze kukaa salama.
19 Nitakuposa uwe wangu milele;
nitakuposa kwa uadilifu na haki,
kwa upendo na huruma.
20 Nitakuposa kwa uaminifu,
nawe utamkubali Mwenyezi Mungu.

21 “Katika siku ile nitajibu,”
asema Mwenyezi Mungu,
“nitajibu kwa anga,
nazo anga zitajibu kwa nchi;
22 nayo nchi itajibu kwa nafaka,
divai mpya na mafuta,
navyo vitajibu kwa Yezreeli.
23 Nitampanda katika nchi kwa ajili yangu mwenyewe;
nami nitaonesha pendo langu kwake

† **2:16** *Mume wangu* Kiebrania ni *Ishi* ‡ **2:16** *Bwana wangu* Kiebrania ni *Baal*

yule ambaye nilimwita, 'Si Mpendwa
Wangu§.'
Nitawaambia wale walioitwa, 'Sio Watu Wangu*,'
'Ninyi ni Watu Wangu';
nao watasema, 'Wewe ndiwe Mungu
wangu'."

# 3

## *Upatanisho wa Hosea na mkewe*

1 Mwenyezi Mungu akaniambia, "Nenda,
ukaoneshe upendo wako kwa mke wako
tena, ingawa amependwa na mwingine naye
ni mzinzi. Mpende kama Mwenyezi Mungu
apendavyo Waisraeli, ingawa wanageukia
miungu mingine na kupenda mikate mitamu
ya zabibu kavu iliyowekwa wakfu."
2 Basi nilimnunua huyo mwanamke kwa
shekeli kumi na tano* za fedha, pia kwa kiasi
kama cha homeri moja na nusu† ya shayiri.
3 Kisha nilimwambia, "Utaishi nami kwa siku
nyingi, hupaswi kuwa kahaba au kuwa na uhu-
siano wa karibu na mtu yeyote, nami nitaishi na
wewe."
4 Kwa maana Waisraeli wataishi siku nyingi
bila kuwa na mfalme wala mkuu, bila kuwa
na dhabihu wala mawe matakatifu, bila kizibau
wala miungu ya nyumbani.
5 Baadaye Waisraeli watarudi na kumtafuta
Mwenyezi Mungu, Mungu wao, na Daudi mfalme

§ **2:23** Kiebrania ni *Lo-Ruhama* (taz. 1:6). * **2:23** Kiebrania ni *Lo-Ami* (taz. 1:9). * **3:2** Shekeli 15 ni sawa na gramu 170. † **3:2** Homeri moja na nusu ni kama lita 330.

wao. Watakuja wakitetemeka kwa Mwenyezi Mungu na kwa baraka zake katika siku za mwisho.

# 4

*Shtaka dhidi ya Israeli*

1 Sikieni neno la Mwenyezi Mungu, enyi Waisraeli,
kwa sababu Mwenyezi Mungu analo shtaka
dhidi yenu ninyi mnaoishi katika nchi:
“Hakuna uaminifu, hakuna upendo,
hakuna kumjua Mungu katika nchi.
2 Kuna kulaani tu, uongo na uuaji,
wizi na uzinzi,
bila kuwa na mipaka,
nao umwagaji damu mmoja
baada ya mwingine.
3 Kwa sababu hii nchi huomboleza,
wote wanaoishi ndani yake wanadhoofika;
wanyama wa kondeni, ndege wa angani
na samaki wa baharini wanakufa.

4 “Lakini mtu yeyote na asilete shtaka,
mtu yeyote na asimlaumu mwenzake,
kwa maana watu wako ni kama wale
waletao mashtaka dhidi ya kuhani.
5 Unajikwaa usiku na mchana,
nao manabii hujikwaa pamoja nawe.
Kwa hiyo nitamwangamiza mama yako:
6 watu wangu wanaangamizwa
kwa kukosa maarifa.

“Kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa,

mimi nami nitakukataa wewe
usiwe kuhani kwangu mimi;
kwa kuwa umeacha kuijali Torati ya Mungu wako
mimi nami sitawajali watoto wako.
7 Kadiri makuhani walivyoongezeka,
ndivyo walivyozidi kutenda dhambi dhidi yangu,
walibadilisha utukufu wao kwa kitu cha aibu.
8 Wanajilisha dhambi za watu wangu
na kupendezwa na uovu wao.
9 Hata itakuwa: Kama walivyo watu,
ndivyo walivyo makuhani.
Nitawaadhibu wote wawili kwa ajili ya njia zao
na kuwalipa kwa matendo yao.

10 "Watakula lakini hawatashiba;
watajiingiza katika ukahaba
lakini hawataongezeka,
kwa sababu wamemwacha Mwenyezi Mungu
na kujiingiza wenyewe
11 katika ukahaba;
kunywa divai ya zamani na divai mpya
huondoa ufahamu
12 wa watu wangu.
Hutaka shauri kutoka kwa sanamu ya mti
nao hujibiwa na fimbo ya mti.
Roho ya ukahaba imewapotosha,
hawana uaminifu kwa Mungu wao.
13 Wanatoa dhabihu juu ya vilele vya milima
na sadaka za kuteketezwa juu ya vilima,
chini ya mialoni, milibua na miela,
ambako kuna vivuli vizuri.

Kwa hiyo binti zenu wamegeukia ukahaba
na wake za wana wenu uzinzi.

14 “Sitawaadhibu binti zenu wakati
wanapogeukia ukahaba,
wala wake za wana wenu
wanapofanya uzinzi,
kwa sababu wanaume wenyewe huandamana na malaya
na kutambikia pamoja na makahaba
wa mahali pa ibada za sanamu:
watu wasiokuwa na ufahamu
wataangamia!

15 “Ingawa umefanya uzinzi, ee Israeli,
Yuda naye asije akawa na hatia.

“Usiende Gilgali,
usipande kwenda Beth-Aveni*.
Wala usiape,
‘Hakika kama Mwenyezi Mungu aishivyo!’
16 Waisraeli ni wakaidi,
kama ndama jike mkaidi.
Ni jinsi gani basi Mwenyezi Mungu anaweza kuwachunga
kama wana-kondoo
katika shamba la majani?
17 Efraimu amejiunga na sanamu,
achana naye!
18 Hata wakati wamemaliza vileo vyao
wanaendelea na ukahaba wao,
watawala wao hupenda sana

---

* **4:15** maana yake *Nyumba ya Ubatili* (au *Uovu*); yaani *Betheli* kwa dhihaka

njia za aibu.
19 Kisulisuli kitawafagilia mbali
na dhabihu zao zitawaletea aibu.

# 5

*Hukumu dhidi ya Israeli*

1 “Sikieni hili, enyi makuhani!
Kuweni wasikivu, enyi Waisraeli!
Sikieni, ee nyumba ya mfalme!
Hukumu hii ni dhidi yenu:
Mmekuwa mtego huko Mispa,
wavu uliotandwa juu ya Tabori.
2 Waasi wamezidisha sana mauaji.
Mimi nitawatiisha wote.
3 Ninajua yote kuhusu Efraimu,
Israeli hukufichika kwangu.
Efraimu, sasa umegeukia ukahaba,
Israeli amenajisika.

4 “Matendo yao hayawaachii
kurudi kwa Mungu wao.
Roho ya ukahaba iko ndani ya mioyo yao,
hawamkubali Mwenyezi Mungu.
5 Kiburi cha Israeli kinashuhudia dhidi yao;
Waisraeli, hata Efraimu,
wanajikwaa katika dhambi zao;
pia Yuda atajikwaa pamoja nao.
6 Wanapoenda na makundi yao ya kondoo na ng’ombe
kumtafuta Mwenyezi Mungu,
hawatampata;
yeye amejiondoa kutoka kwao.
7 Wao si waaminifu kwa Mwenyezi Mungu;

wamezaa watoto haramu.
Sasa sikukuu zao za Mwandamo wa Mwezi
zitawaangamiza wao
pamoja na mashamba yao.

8 “Pigeni tarumbeta huko Gibea,
na baragumu huko Rama.
Pazeni kelele za vita huko Beth-Aveni*;
ongoza, ee Benyamini.
9 Efraimu ataachwa ukiwa
katika siku ya kuadhibiwa.
Miongoni mwa makabila ya Israeli
ninatangaza lile ambalo halina budi kutukia.
10 Viongozi wa Yuda ni kama wale
wanaosogeza mawe ya mpaka.
Nitamwaga ghadhabu yangu juu yao
kama mafuriko ya maji.
11 Efraimu amedhulumiwa,
amekanyagwa katika hukumu
kwa kuwa amekusudia kufuatia sanamu.
12 Mimi ni kama nondo kwa Efraimu,
na kama uozo kwa watu wa Yuda.

13 “Efraimu alipoona ugonjwa wake,
naye Yuda vidonda vyake,
ndipo Efraimu aligeukia Ashuru,
na kuomba msaada kwa mfalme mkuu.
Lakini hawezi kukuponya,
hawezi kukuponya vidonda vyako.
14 Kwa maana nitakuwa kama simba kwa Efraimu,
kama simba mkubwa kwa Yuda.

* **5:8** maana yake *Nyumba ya Ubatili* (au *Uovu*); yaani *Betheli* kwa dhihaka

Nitawararua vipande vipande na kuondoka;
nitawachukua mbali,
na hakuna wa kuwaokoa.
15 Kisha nitarudi mahali pangu
hadi watakapokubali kosa lao.
Nao watautafuta uso wangu;
katika taabu yao watanitafuta kwa bidii."

# 6

*Israeli asiye tubu*

1 "Njooni, tumrudie Mwenyezi Mungu.
Ameturarua vipande vipande
lakini atatuponya;
ametujeruhi lakini
atatufunga majeraha yetu.
2 Baada ya siku mbili atatufufua;
katika siku ya tatu atatuinua,
ili tuweze kuishi mbele zake.
3 Tumkubali Mwenyezi Mungu,
tukaze kumkubali yeye.
Kutokea kwake ni hakika kama vile
kuchomoza kwa jua;
atatujia kama mvua za masika,
kama vile mvua za vuli
ziinyweshavyo nchi."

4 "Nifanye nini nawe, Efraimu?
Nifanye nini nawe, Yuda?
Upendo wako ni kama ukungu wa asubuhi,
kama umande wa alfajiri utowekao.
5 Kwa hiyo nimewakata ninyi vipande vipande
nikitumia manabii wangu;
nimewaua ninyi kwa maneno ya kinywa changu,

hukumu zangu zinawaka
kama umeme juu yenu.
6 Kwa maana nataka rehema, wala si dhabihu,
na kumkubali Mungu
kuliko sadaka za kuteketezwa.
7 Wamevunja agano kama Adamu:
hawakuwa waaminifu kwangu huko.
8 Gileadi ni mji wa watenda maovu,
umetiwa madoa kwa nyayo za damu.
9 Kama wanyang'anyi wamviziavyo mtu,
ndivyo magenge ya makuhani wafanyavyo;
wanaulia watu kwenye njia iendayo Shekemu,
wakifanya uhalifu wa aibu.
10 Nimeona jambo la kutisha
katika nyumba ya Israeli.
Huko Efraimu amejitolea kwa ukahaba
na Israeli amenajisika.

11 "Pia kwa ajili yako, Yuda,
mavuno yameamriwa.

"Wakati wowote ningerejesha neema ya watu wangu,

# 7

1 kila mara nilipotaka kumponya Israeli,
dhambi za Efraimu zinafichuliwa
na maovu ya Samaria yanafunuliwa.
Wanafanya udanganyifu,
wezi huvunja nyumba,
maharamia hunyang'anya barabarani,
2 lakini hawafahamu kwamba
ninakumbuka matendo yao yote mabaya.

Dhambi zao zimewameza,
ziko mbele zangu siku zote.

3 “Wanamfurahisha sana mfalme kwa maovu yao,
wakuu wao kwa uongo wao.
4 Wote ni wazinzi,
wanawaka kama tanuru
ambalo moto wake mwokaji hana haja ya kuuchochea
kuanzia kukanda unga
hadi umekwisha kuumuka.
5 Katika sikukuu ya mfalme wetu
wakuu wanawaka kwa mvinyo,
naye anawaunga mkono wenye mizaha.
6 Mioyo yao ni kama tanuru,
wanamwendea kwa hila.
Hasira yao inafoka moshi usiku kucha,
wakati wa asubuhi inalipuka
kama miali ya moto.
7 Wote ni moto kama tanuru;
wanawaangamiza watawala wao.
Wafalme wake wote wanaanguka,
wala hakuna yeyote kati yao aniitaye mimi.

8 “Efraimu anajichanganya na mataifa;
Efraimu ni mkate ambao haukuiva.
9 Wageni wananyonya nguvu zake,
lakini hafahamu hilo.
Nywele zake zina mvi hapa na pale,
lakini hana habari.
10 Kiburi cha Israeli kinashuhudia dhidi yake,
lakini pamoja na haya yote
harudi kwa Mwenyezi Mungu, Mungu wake,

wala kumtafuta.

11 “Efraimu ni kama hua,
hudanganywa kwa urahisi na hana akili:
mara anaita Misri,
mara anageukia Ashuru.
12 Watakapoenda, nitatupa wavu wangu juu yao;
nitawavuta chini waanguke kama ndege wa angani.
Nitakaposikia wakikusanyika pamoja,
nitawanasa.
13 Ole wao, kwa sababu
wamepotoka kutoka kwangu!
Maangamizi ni yao
kwa sababu wameniasi!
Ninatamani kuwakomboa,
lakini wanasema uongo dhidi yangu.
14 Hawanililii mimi kutoka mioyoni mwao,
bali wanaomboleza vitandani mwao.
Hukusanyika pamoja kwa ajili ya nafaka na divai mpya,
lakini hugeukia mbali nami.
15 Niliwafundisha na kuwatia nguvu,
lakini wanapanga mabaya dhidi yangu.
16 Hawamgeukii Yeye Aliye Juu Sana,
wako kama upinde wenye kasoro.
Viongozi wao wataanguka kwa upanga
kwa sababu ya maneno yao ya jeuri.
Kwa ajili ya hili watadhihakiwa
katika nchi ya Misri.

# 8

*Israeli kuvuna kisulisuli*

1 “Wekeni tarumbeta midomoni mwenu!

Tai yuko juu ya nyumba ya Mwenyezi Mungu
kwa sababu watu wamevunja agano langu,
wameasi dhidi ya sheria yangu.
2 Israeli ananililia,
‘Ee Mungu wetu, tunakukubali!’
3 Lakini Israeli amekataa lile lililo jema,
adui atamfuatia.
4 Wanaweka wafalme bila idhini yangu,
wamechagua wakuu bila kibali changu.
Kwa fedha zao na dhahabu
wamejitengenezea sanamu kwa ajili
ya maangamizi yao wenyewe.
5 Ee Samaria, tupilieni mbali sanamu yenu ya ndama!
Hasira yangu inawaka dhidi yao.
Watakuwa najisi hadi lini?
6 Zimetoka katika Israeli!
Ndama huyu: ametengenezwa na fundi, si Mungu.
Atavunjwa vipande vipande,
yule ndama wa Samaria.

7 “Wanapanda upepo
na kuvuna kisulisuli.
Bua halina suke,
halitatoa unga.
Kama lingetoa nafaka,
wageni wangeila yote.
8 Israeli amemezwa;
sasa yupo miongoni mwa mataifa
kama kitu kisicho na thamani.
9 Kwa kuwa wamepanda kwenda Ashuru
kama punda-mwitu anayetangatanga peke yake.

Efraimu amejiuza mwenyewe
kwa wapenzi.
10 Ingawa wamejiuza wenyewe miongoni mwa mataifa,
sasa nitawakusanya pamoja.
Wataanza kudhoofika chini ya uonevu
wa mfalme mwenye nguvu.

11 “Ingawa Efraimu alijenga madhabahu nyingi
kwa ajili ya sadaka za dhambi,
hizi zimekuwa madhabahu
za kufanyia dhambi.
12 Niliwaandikia mambo mengi yaliyohusu sheria yangu,
lakini waliziangalia kama kitu kigeni.
13 Wanatoa dhabihu nilizopewa mimi
nao wanakula hiyo nyama,
lakini Mwenyezi Mungu hapendezwi nao.
Sasa ataukumbuka uovu wao
na kuadhibu dhambi zao:
Watarudi Misri.
14 Israeli amemsahau Muumba wake
na kujenga majumba ya kifalme,
Yuda amejengea miji mingi ngome.
Lakini nitatuma moto kwenye miji yao
utakaoteketeza ngome zao.”

# 9

*Adhabu kwa Israeli*

1 Usifurahie, ee Israeli;
usishangilie kama mataifa mengine.
Kwa kuwa hukuwa
mwaminifu kwa Mungu wako;
umependa ujira wa kahaba kwenye kila sakafu

ya kupuria nafaka.
2 Sakafu za kupuria nafaka na mashinikizo ya kukamulia divai
havitalisha watu,
divai mpya itawapungukia.
3 Hawataishi katika nchi ya Mwenyezi Mungu,
Efraimu atarudi Misri
na atakula chakula
kilicho najisi huko Ashuru.
4 Hawatammiminia Mwenyezi Mungu sadaka ya divai
wala dhabihu zao hazitampendeza.
Dhabihu kama hizo zitakuwa kwao
kama mkate wa waombolezaji;
nao wote wazilao watakuwa najisi.
Chakula hiki kitakuwa kwa ajili yao wenyewe;
kisije katika Hekalu la Mwenyezi Mungu.

5 Mtafanya nini katika siku ya sikukuu zenu zilizoamriwa,
katika siku za sikukuu za Mwenyezi Mungu?
6 Hata ikiwa wataokoka maangamizi,
Misri atawakusanya,
nayo Memfisi* itawazika.
Hazina zao za fedha zitasongwa na michongoma,
nayo miiba itafunika mahema yao.
7 Siku za adhabu zinakuja,
siku za malipo zimewadia.
Israeli na afahamu hili.
Kwa sababu dhambi zenu ni nyingi sana
na uadui wenu ni mkubwa sana,
nabii anadhaniwa ni mpumbavu,
mtu aliyeongozwa na Mungu

* **9:6** yaani *Nofu*

anaonekana mwendawazimu.
8 Nabii, pamoja na Mungu wangu,
ndiye mlinzi juu ya Efraimu,
hata hivyo mitego inamngojea
katika mapito yake yote,
na uadui katika nyumba ya Mungu wake.
9 Wamezama sana katika rushwa,
kama katika siku za Gibea.
Mungu atakumbuka uovu wao
na kuwaadhibu kwa ajili ya dhambi zao.

10 “Nilipompata Israeli, ilikuwa kama
kupata zabibu jangwani;
nilipowaona baba zenu, ilikuwa kama kuona
matunda ya kwanza katika mtini.
Lakini walipofika Baal-Peori, walijiweka wakfu
kwa ile sanamu ya aibu,
nao wakawa najisi
kama kitu kile walichokipenda.
11 Utukufu wa Efraimu utaruka kama ndege:
hakuna kuzaa, hakuna kubeba mimba,
hakuna kuchukua mimba.
12 Hata wakilea watoto,
nitamuua kila mmoja.
Ole wao
nitakapowapiga kisogo!
13 Nimemwona Efraimu, kama Tiro,
aliyeoteshwa mahali pazuri.
Lakini Efraimu wataleta
watoto wao kwa mchinjaji.”

14 Wape, Ee Mwenyezi Mungu,
je, utawapa nini?
Wape tumbo zinazoharibu mimba

na matiti yaliyokauka.

15 “Kwa sababu ya uovu wao wote huko Gilgali,
niliwachukia huko.
Kwa sababu ya matendo yao ya dhambi,
nitawafukuza katika nyumba yangu.
Sitawapenda tena,
viongozi wao wote ni waasi.
16 Efraimu ameharibiwa,
mzizi wao umenyauka,
hawazai tunda.
Hata kama watazaa watoto,
nitawachinja wazao wao
waliotunzwa vizuri.”

17 Mungu wangu atawakataa
kwa sababu hawakumtii;
watakuwa watu wa kutangatanga
miongoni mwa mataifa.

# 10

1 Israeli alikuwa mzabibu uliostawi sana,
alijizalia matunda mwenyewe.
Kadiri matunda yake yalivyoongezeka,
alijenga madhabahu zaidi;
kadiri nchi yake ilivyostawi,
alipamba mawe yake ya ibada.
2 Moyo wao ni mdanganyifu,
nao sasa lazima wachukue hatia yao.
Mwenyezi Mungu atabomoa madhabahu zao
na kuharibu mawe yao ya ibada.

3 Kisha watasema, “Hatuna mfalme

kwa sababu hatukumheshimu Mwenyezi Mungu.
Lakini hata kama tungekuwa na mfalme,
angeweza kutufanyia nini?”
4 Wanaweka ahadi nyingi,
huapa viapo vya uongo
wanapofanya mapatano;
kwa hiyo mashtaka huchipuka
kama magugu ya sumu
katika shamba lililolimwa.
5 Watu wanaoishi Samaria huogopa
kwa ajili ya sanamu ya ndama ya Beth-Aveni*.
Watu wake wataiombolezea,
vivyo hivyo kuhani wake wa kuabudu sanamu,
wale waliokuwa wamefurahia fahari yake,
kwa sababu itaondolewa kutoka kwao
kwenda uhamishoni.
6 Itachukuliwa kwenda Ashuru
kama ushuru kwa mfalme mkuu.
Efraimu atafedheheshwa;
Israeli ataaibika kwa ajili ya sanamu zake za mti.
7 Samaria na mfalme wake wataelea
kama kijiti juu ya maji.
8 Mahali pa juu pa uovu† pataharibiwa:
ndiyo dhambi ya Israeli.
Miiba na mibaruti itaota
na kufunika madhabahu zao.
Kisha wataiambia milima, “Tufunikeni!”
na vilima, “Tuangukieni!”

* **10:5** maana yake *Nyumba ya Ubatili* (au *Uovu*); yaani *Betheli* kwa dhihaka † **10:8** yaani *Aveni* kwa Kiebrania, kumaanisha *Beth-Aveni*

9 “Tangu siku za Gibea, umetenda dhambi, ee Israeli,
huko ndiko ulibaki.
Je, vita havikuwapata
watenda maovu huko Gibea?
10 Wakati nitakapopenda, nitawaadhibu;
mataifa yatakusanywa dhidi yao
ili kuwaweka katika vifungo
kwa ajili ya dhambi zao mbili.
11 Efraimu ni ndama jike aliyefundishwa
ambaye hupenda kupura;
hivyo nitamfunga nira
juu ya shingo yake nzuri.
Nitamwendesha Efraimu,
Yuda lazima alime,
naye Yakobo lazima avunjavunje
mabonge ya udongo.
12 Jipandieni wenyewe haki,
vuneni matunda ya upendo usio na kikomo,
vunjeni ardhi yenu isiyolimwa;
kwa kuwa ni wakati wa kumtafuta Mwenyezi Mungu,
hadi atakapokuja
na kuwanyeshea juu yenu haki.
13 Lakini mmepanda uovu,
mkavuna ubaya,
mmekula tunda la udanganyifu.
Kwa sababu mmetegemea nguvu zenu wenyewe
na wingi wa mashujaa wenu,
14 mngurumo wa vita utainuka dhidi ya watu wako,
na ngome zako zote zitaharibiwa:

kama Shalmani alivyoharibu Beth-Arbeli katika
siku ile ya vita,
wakati mama pamoja na watoto wao
walipotupwa kwa nguvu ardhini.
15 Ndivyo itakavyotokea kwako, ee Betheli,
kwa sababu uovu wako ni mkuu.
Siku ile itakapopambazuka,
mfalme wa Israeli ataharibiwa kabisa.

# 11

## *Upendo wa Mwenyezi Mungu kwa Israeli*

1 “Israeli alipokuwa mtoto, nilimpenda;
nilimwita mwanangu kutoka Misri.
2 Lakini kadiri nilivyomwita Israeli,
ndivyo walivyoenda mbali nami.
Walitoa dhabihu kwa Mabaali
na kufukiza uvumba kwa vinyago.
3 Mimi ndiye niliyemfundisha Efraimu kutembea,
nikiwashika mikono;
lakini hawakutambua
kuwa ni mimi niliyewaponya.
4 Niliwaongoza kwa kamba za huruma ya kibinadamu,
kwa vifungo vya upendo;
niliondoa nira shingoni mwao
nami nikainama kuwalisha.

5 “Je, hawatarudi Misri,
nayo Ashuru haitawatawala
kwa sababu wamekataa kutubu?
6 Upanga utavurumishwa katika miji yao,
nao utaharibu makomeo ya malango yao
na kukomesha mipango yao.

7 Watu wangu wamedhamiria kuniacha.
Hata wakimwita Yeye Aliye Juu Sana,
kwa vyovyote hatawainua.

8 “Efraimu, ninawezaje kukuacha?
Ee Israeli, ninawezaje kukutoa?
Nitawezaje kukutendea kama Adma?
Nitawezaje kukufanya kama Seboimu?
Moyo wangu umegeuka ndani yangu,
huruma zangu zote zimeamshwa.
9 Sitatimiza hasira yangu kali,
wala sitageuka na kumharibu Efraimu.
Kwa kuwa mimi ndimi Mungu,
wala si mwanadamu,
Aliye Mtakatifu miongoni mwenu.
Sitakuja kwa ghadhabu.
10 Watamfuata Mwenyezi Mungu;
atanguruma kama simba.
Anapounguruma,
watoto wake watakuja wakitetemeka
kutoka magharibi.
11 Watakuja wakitetemeka
kama ndege wakitoka Misri,
kama hua wakitoka Ashuru.
Nitawafanya waishi katika nyumba zao,”
asema Mwenyezi Mungu.

*Dhambi ya Israeli*

12 Efraimu amenizunguka kwa uongo,
nyumba ya Israeli kwa udanganyifu.
Naye Yuda ni mkaidi dhidi ya Mungu,
hata kinyume cha yule mwaminifu Aliye Mtakatifu.

# 12

1 Efraimu anajilisha upepo;
hufukuzia upepo wa mashariki kutwa nzima
na kuzidisha uongo na jeuri.
Anafanya mkataba na Ashuru
na kutuma mafuta ya zeituni Misri.
2 Mwenyezi Mungu analo shtaka dhidi ya Yuda,
atamwadhibu Yakobo kwa kadiri ya njia zake
na kumlipa kwa kadiri ya matendo yake.
3 Yakobo akiwa tumboni alishika kisigino cha kaka yake;
kama mwanadamu, alishindana na Mungu.
4 Alishindana na malaika na kumshinda;
alilia na kuomba upendeleo wake.
Alimkuta huko Betheli
na kuzungumza naye huko:
5 Bwana Mwenyezi Mungu,
Mungu wa majeshi ya mbinguni,
Mwenyezi Mungu ndilo jina lake!
6 Lakini ni lazima urudi kwa Mungu wako;
dumisha upendo na haki,
nawe umngojee Mungu wako siku zote.

7 Mfanyabiashara hutumia vipimo vya udanganyifu;
hupenda kupunja.
8 Efraimu hujisifu akisema,
"Mimi ni tajiri sana; nimetajirika.
Pamoja na utajiri wangu wote hawatakuta ndani yangu
uovu wowote au dhambi."

9 “Mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wenu,
niliyewaleta kutoka Misri;
nitawafanya mkae tena kwenye mahema,
kama vile katika siku
za sikukuu zenu zilizoamriwa.
10 Niliongea na manabii, nikawapa maono mengi
na kusema mifano kupitia wao.”

11 Je, Gileadi si mwovu?
Watu wake hawafai kitu!
Je, hawatoi dhabihu za mafahali huko Gilgali?
Madhabahu zao zitakuwa
kama malundo ya mawe
katika shamba lililolimwa.
12 Yakobo alikimbilia katika nchi ya Aramu;
Israeli alitumika ili apate mke,
ili aweze kulipa kwa ajili yake alichunga kondoo.
13 Mwenyezi Mungu alimtumia nabii
kumpandisha Israeli kutoka Misri,
kupitia kwa nabii alimtunza.
14 Lakini Efraimu amemchochea sana hasira;
Bwana wake ataleta juu yake
hatia yake ya kumwaga damu naye atamlipiza
kwa ajili ya dharau yake.

# 13

## *Hasira ya Mwenyezi Mungu dhidi ya Israeli*

1 Efraimu alipozungumza, watu walitetemeka;
alitukuzwa katika Israeli.
Lakini alikuwa na hatia ya kumwabudu Baali,
naye akafa.
2 Sasa wanatenda dhambi zaidi na zaidi;
wanajitengenezea sanamu

kutokana na fedha yao,
vinyago vilivyotengenezwa kwa uhodari,
vyote kazi ya fundi stadi.
Inasemekana kuhusu hawa watu,
“Hutoa dhabihu za binadamu
na kubusu sanamu za ndama.”
3 Kwa hiyo watakuwa kama ukungu wa asubuhi,
kama umande wa alfajiri utowekao,
kama makapi yapeperushwayo
kutoka sakafu ya kupuria nafaka,
kama moshi utorokao kupitia dirishani.

4 “Bali mimi ndimi Mwenyezi Mungu, Mungu wenu,
niliyewaleta ninyi toka Misri.
Msimkubali Mungu mwingine ila mimi,
hakuna Mwokozi isipokuwa mimi.
5 Niliwatunza huko jangwani,
katika nchi yenye joto liunguzalo.
6 Nilipowalisha, walishiba,
waliposhiba, wakajivuna,
kisha wakanisahau mimi.
7 Kwa hiyo nitakuja juu yao kama simba,
kama chui nitawavizia kando ya njia.
8 Kama dubu aliyenyang’anywa watoto wake,
nitawashambulia na kurarua vifua vyenu.
Kama simba nitawala;
mnyama pori atawararua vipande vipande.

9 “Ee Israeli, umeangamizwa,
kwa sababu wewe u kinyume nami,
kinyume na msaidizi wako.
10 Yuko wapi mfalme wako,

ili apate kukuokoa?
Wako wapi watawala wako katika miji yako yote
ambao ulisema kuwahusu,
‘Nipe mfalme na wakuu’?
11 Hivyo katika hasira yangu nilikupa mfalme
na katika ghadhabu yangu nilimwondoa.
12 Kosa la Efraimu limehifadhiwa,
dhambi zake zimewekwa katika kumbukumbu.
13 Uchungu kama wa mwanamke anayejifungua mtoto humjia,
lakini yeye ni mtoto asiyekuwa na hekima;
wakati utakapowadia hatatoka
katika tumbo la mama yake.

14 “Nitawakomboa watu hawa kutoka nguvu za kaburi,
nitawakomboa kutoka mautini.
Yako wapi, ee mauti, mateso yako?
Uko wapi, ee Kuzimu*, uharibifu wako?

“Sitakuwa na huruma,
15 hata ingawa Efraimu atastawi
miongoni mwa ndugu zake.
Upepo wa mashariki kutoka kwa Mwenyezi Mungu utakuja,
ukivuma kutoka jangwani,
chemchemi yake haitatoa maji
na kisima chake kitakauka.
Ghala lake litatekwa
hazina zake zote.
16 Watu wa Samaria ni lazima wabebe hatia yao,

* **13:14** Kuzimu kwa Kiebrania ni *Sheol*, yaani *Shimo lisilo na mwisho.*

kwa sababu wameasi dhidi ya Mungu wao.
Wataanguka kwa upanga;
watoto wao wadogo watatupwa kwa nguvu ardhini,
wanawake wao walio na mimba watatumbuliwa."

# 14

*Toba iletayo baraka*

1 Rudi, ee Israeli, kwa Mwenyezi Mungu, Mungu wako.
Dhambi zako zimekuwa anguko lako!
2 Chukueni maneno pamoja nanyi,
mkamrudie Mwenyezi Mungu.
Mwambieni:
"Samehe dhambi zetu zote
na utupokee kwa neema,
ili tuweze kutoa matunda yetu
kama sadaka za mafahali.
3 Ashuru hawezi kutuokoa,
hatutapanda farasi wa vita.
Kamwe hatutasema tena 'miungu yetu'
kwa kile ambacho mikono yetu wenyewe imetengeneza,
kwa kuwa kwako wewe yatima hupata huruma."

4 "Nitaponya ukaidi wao
na kuwapenda kwa hiari yangu,
kwa kuwa hasira yangu imeondoka kwao.
5 Nitakuwa kama umande kwa Israeli;
atachanua kama yungiyungi.
Kama mwerezi wa Lebanoni
atashusha mizizi yake chini;

6 matawi yake yatatanda.
Fahari yake itakuwa kama mti wa mzeituni,
harufu yake nzuri kama mwerezi wa Lebanoni.
7 Watu wataishi tena kwenye kivuli chake.
Atastawi kama nafaka.
Atachanua kama mzabibu,
nao umaarufu wake utakuwa
kama divai inayotoka Lebanoni.
8 Ee Efraimu, nina shughuli gani tena na sanamu?
Nitamjibu na kumtunza.
Mimi ni kama msunobari wenye majani mabichi;
kuzaa kwako matunda kunatoka kwangu."

9 Ni nani mwenye hekima? Atayatambua mambo haya.
Ni nani mwenye ufahamu? Huyu atayaelewa.
Njia za Mwenyezi Mungu ni adili;
wenye haki huenda katika njia hizo,
lakini waasi watajikwaa ndani yake.

# Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu

## The Holy Bible in Swahili: Open Neno: Maandiko Matakatifu 2024

copyright © 2018, 2024 Biblica, Inc.

Language: Kiswahili (Swahili)

Contributor: Biblica, Inc.

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

**Creative Commons License**

Kazi hii imewezeshwa kupitia idhini ya kundi la the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). Ili kuona nakala ya idhini hii, angalia kwenye anwani tovuti ya http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 au uandike barua kwa Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® ni alama ya biashara iliyosajilishwa na shirika la Biblica, Inc; unahitaji ruhusa ya kimaandiko kutoka kwa Biblica, Inc. ili kutumia alama ya biashara ya Biblica®. Kulingana na makubaliano ya leseni ya CC BY-SA, unaweza kutoa nakala na kusambaza kazi hii bila kuibadilisha kamwe, mradi tu udumishe alama ya biashara ya Biblica®. Ukibadilisha au kufasiri kazi hii, na hivyo ukanyambua kazi tofauti, sharti uondoe alama ya biashara ya Biblica®. Katika kazi uliyonyambua, sharti uarifu mabadiliko yako, na kutambua kazi yako hivi: "Kazi ya asili ya Biblica, Inc. inapatikana bila bei katika tovuti zawww.biblica.com na open.bible."

Ilani ya hakimiliki sharti iwe katika ukurasa wa kichwa au wa hakilimiliki kama ifuatavyo:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™
Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.
Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™
Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

Sharti pia uwasilishe kazi uliyonyambua kupitia kwa liseni hiyo hiyo ya CC BY-SA.

Ikiwa ungependa kujulisha Biblica, Inc. kuhusu tafsiri yako ya kazi hii, tafadhali wasiliana nasi katika tovuti https://open.bible/contact-us.

This work is made available under the Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-SA). To view a copy of this license, visit http://creativecommons.org/licenses/by-sa/4.0 or send a letter to Creative Commons, PO Box 1866, Mountain View, CA 94042, USA.

Biblica® is a trademark registered by Biblica, Inc., and use of the Biblica® trademark requires the written permission of Biblica, Inc. Under the terms of the CC BY-SA license, you may copy and redistribute this unmodified work as long as you keep the Biblica® trademark intact. If you modify a copy or translate this work, thereby creating a derivative work, you must remove the Biblica® trademark. On the derivative work, you must indicate what changes you have made and attribute the work as follows: "The original work by Biblica, Inc. is available for free atwww.biblica.com and open.bible."

Notice of copyright must appear on the title or copyright page of the work as follows:

Biblica® Toleo Wazi Neno: Maandiko Matakatifu™ ONMM™

Hakimiliki © 2018, 2024 na Biblica, Inc.

Biblica® Open Kiswahili Contemporary Scriptures™

Copyright © 2018, 2024 by Biblica, Inc.

"Biblica" ni alama ya biashara iliyosajiliwa katika United States Patent and Trademark Office (ofisi ya hataza na alama za biashara Marekani) na shirika la Biblica, Inc. Imetumiwa na ruhusa.

"Biblica" is a trademark registered in the United States Patent and Trademark Office by Biblica, Inc. Used with permission.

You must also make your derivative work available under the same license (CC BY-SA).

If you would like to notify Biblica, Inc. regarding your translation of this work, please contact us at https://open.bible/contact-us.

This translation is made available to you under the terms of the Creative Commons Attribution Share-Alike license 4.0.

You have permission to share and redistribute this Bible translation in any format and to make reasonable revisions and adaptations of this translation, provided that:

You include the above copyright and source information.

If you make any changes to the text, you must indicate that you did so in a way that makes it clear that the original licensor is not necessarily endorsing your changes.
If you redistribute this text, you must distribute your contributions under the same license as the original.

Pictures included with Scriptures and other documents on this site are licensed just for use with those Scriptures and documents. For other uses, please contact the respective copyright owners.

Note that in addition to the rules above, revising and adapting God's Word involves a great responsibility to be true to God's Word. See Revelation 22:18-19.

2025-05-21

---

PDF generated using Haiola and XeLaTeX on 20 May 2025 from source files dated 21 May 2025
72687ba8-7233-577d-bf23-786df16f869d